**HOTUBA YA MHE. MUSSA AZZAN ZUNGU, WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA), KATIKA UZINDUZI WA KAMATI YA KITAIFA YA USIMAMIZI WA MATUMIZI SALAMA YA BIOTEKNOLOJIA YA KISASA, JENGO LA LAPF MAKOLE, DODOMA,**

**12 – 13 AGOSTI, 2020**

***Ndugu wana Kamati,***

***Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais,***

***Ndugu Wageni Waalikwa,***

***Wanahabari,***

***Mabibi na Mabwana.***

Awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia afya na kutuwezesha kukutana hapa leo. Aidha, nichukue kutumia fursa hii kuwakaribisha wajumbe wa Kamati ya Kitaifa ya Usimamizi wa Matumizi Salama ya Bioteknolojia ya Kisasa katika hafla hii ya uzinduzi wa Kamati hii muhimu. Pamoja na uzinduzi wa Kamati yenu, hafla hii inatoa fursa kwa wajumbe kufahamiana na kujadiliana kwa pamoja namna bora ya kutekeleza wajibu na majukumu yenu. Kushiriki kwenu katika uzinduzi huu ni kielelezo tosha cha umuhimu mliouweka katika usimamizi wa matumizi salama ya bioteknolojia ya kisasa.

***Ndugu wana Kamati,***

Kama mnavyofahamu, Tanzania imeridhia Itifaki ya Cartagena *(The Cartagena Protocol on Biosafety)* mwaka 2003 na Itifaki ya Ziada ya Nagoya

Kuala Lumpur mwaka 2019 kwa lengo la kusimamia matumizi salama ya biotekinolojia ya kisasa na uwajibikaji kisheria na fidia kwa madhara yanayoweza kutokea kutokana na matumizi ya bioteknolojia ya kisasa.

Katika kutekeleza matakwa ya Itifaki hizo Serikali iliandaa Kanuni ya Usimamizi wa matumizi salama ya biotekinolojia ya kisasa za mwaka 2009 na marekebisho yake ya mwaka 2015. Aidha, Kifungu cha 9 cha Kanuni hizo, kimenipa mamlaka ya kuteua wajumbe wa Kamati watakaohudumu kwa kipindi cha miaka mitatu (3). Kwa muktadha huo, nimewateua kuwa wajumbe wa Kamati hii. Hivyo, nichukue fursa hii kuwapongeza wote kwa kuteuliwa kuchukua jukumu hili muhimu kwa taifa letu.

***Ndugu wana Kamati,***

Katika kuhakikisha kunakuwa na usalama na faida ya matumizi ya bioteknolojia ya kisasa, Kamati yenu ina majukumu makubwa ya kuishauri Serikali ikiwa ni pamoja na kupitia maombi ya matumizi ya viumbe na bidhaa zitokanazo na biotejinolojia ya kisasa na kushauri kuhusu Sera, Sheria, tafiti na ushiriki wa sekta binafsi na umma kwa ujumla katika matumizi ya

biotekinolojia ya kisasa. Jukumu hili ni kubwa na linahitaji uzalendo na kujitolea kwa hali ya juu.

Kwa kuzingatia umuhimu wa biotekinolojia ya kisasa na madhara yanayoweza kujitokeza, Serikali imeandaa na kuweka nyenzo mbalimbali za usimamizi wa teknolojia hii ikiwa ni pamoja na: Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004, Mfumo wa Kitaifa wa Usimamizi wa Matumizi Salama ya Bioteknolojia ya Kisasa (*National Biosafety Framework*), 2007; Kanuni za Matumizi Salama ya Bioteknolojia ya Kisasa ya mwaka 2009 (Biosafety Regulation) na marekebisho yake ya mwaka 2015; Miongozo mbalimbali (*Biosafety Guidelines and Mannuals*) za mwaka 2010.

Hadi sasa mfumo wa usimamizi umewezesha kufanyika kwa utafiti ndani ya maabara (Contained) wa mihogo unaolenga kupata ukinzani dhdi ya magonjwa ya virusi vya zao la Muhogo *(Cassava Brown Streak Virus Disease and Cassava Mosaic Virus Disease);* utafiti nje ya maabara *(Confined field trials)* wa mahindi yanayovumilia ukame na Bungua, kusafirisha chakula cha msaada kupitia bandari ya Dar es salaam kwenda nchi jirani.

Hata hivyo, pamoja na hatua hizo bado kuna changamoto mbalimbali zinazokabili eneo hili ikiwa ni pamoja na uelewa mdogo miongoni mwa jamii kuhusu biotekinolojia ya kisasa, uchache wa wataalam wa masuala ya biotekinolojia ya kisasa na usimamizi wake, uhaba wa miundombinu hususan vifaa utambuzi na ung'amuzi wa bidhaa au mazao yatokanayo na biotekinolojia ya kisasa. Hivyo ni mategemeo yangu kuwa, Kamati hii itajielekeleza katika kushauri namna bora ya kukabiliana na changamoto hizi.

Katika kutekeleza majukumu yenu, itakuwa vyema baada ya kikao chenu cha kwanza mkaandaa mpango kazi wa utekelezaji wa mjaukumu yenu kwa kipindi cha miaka mitatu utakaoonesha namna kamati hii itakavyosaidia kuboresha jukumu la kihakikisha kuwa Tanzania inafaidika na matumizi ya tekinolojia hiii kwa maendeleo endelevu.

***Ndugu wana Kamati,***

Nimejulishwa kuwa baada ya ufunguzi huu mtaendelea na warsha ya kukuza uelewa kuhusu masuala ya biotekinolojia ya kisasa ikiwa ni pamoja na faida na changamoto zake. Vile vile mtapata fursa ya kutembelea shamba maalum la utafiti (*Confined Field Trials*) wa mahindi yanayovumilia ukame na bungua

katika kituo cha Utafiti wa Kilimo Makuputora ili kushuhudia shughuli za utafiti kuhusu teknolojia hii.

***Ndugu wana Kamati,***

Mwisho Natoa shukran zangu za dhati kwa Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia *(COSTECH)* kupitia Jukwaa la Bioteknolojia ya Kilimo (*OFAB)* kwa kuendelea kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais katika kuimarisha usimamizi wa matumizi salama ya bioteknolojia ya kisasa nchini hususan kwa utoaji wa mafunzo mbalimbali kwa jamii na wataalam wetu. Aidha, nachukua fursa hii kuwashukuru watoa mada wajumbe wa kaamati, wanahabari na wote walioshiriki kufanikisha hafla hii.

Baada ya kusema hayo, natamka kwamba **Kamati ya Kitaifa ya Matumizi Salama ya Bioteknolojia ya Kisasa imezinduliwa rasmi**.

**Asanteni kwa kunisikiliza.**